EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## Nia na Ridhaa Huru ya Uelewa kabla ya utekelezaji wa mradi (FPIC)

## Kati ya

## Mradi wa Bomba la Mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)

## Na

## Jamii ya Wa-Akie wa Napilukunya, Kiteto

### Utangulizi

Ifuatayo ni Nia na Ridhaa Huru ya Uelewa kabla ya utekelezaji wa mradi (FPIC) kati ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi (EACOP) na jamii ya Wa-Akie wa Napilukunya katika wilaya ya Kiteto, Mkoa wa Manyara , Tanzania inadhihirisha makubaliano ya Ujenzi na utekelezaji wa bomba la mafuta Kwa kuzingatia taratibu za Nia huru na Makubaliano ya ridhaa (FPIC).

Makubaliano haya ya FPIC ni udhihirisho wa namna ya utendaji kazi wa mradi wa EACOP ambao hushirikisha jamii za pembezoni zinazojitambulisha kama jamii za asili ambazo zinaguswa na mradi kwenye Nyanja za kiutamaduni, hivyo kuzipa heshima zinazozingatia haki za binadamu kwa viwango vya kitaifa na kimataifa. Makubaliano haya pia yana dhihirisha jamii hii imekubali na kutoa ridhaa ya kifanyika kwa shughuli za mradi wa EACOP katika jamii yao kama ambavyo inaelezwa katika Mpango wa EACOP wa jamii za pembezoni zinazojitambulisha kama jamii za asili.

### Ahadi za EACOP

EACOP inatoa ahadi kwa jamii ya waakie ( pamoja na jamii nyingine zinazojulikana kama jamii ya pembezoni na inatambulika kama kundi la wazawa asilia)

Kwa kuweka kwenye maandishi katika Mpango wa utelezaji wa mradi , na ulitiwa sahihi na viongozi wa jamii za waakie, wamaasai, wabarabaig, na wataturu tarehe 28 Oktoba mwaka 2021, Arusha, Tanzania. Ahadi hizo ni:

(a) Kushiriki katika kupata ushauri wa kina,

(b) Kujenga uwezo wa jamii,

(c) Kupata njia za kutatua migogoro kwa taratibu za jamii husika,

(d) Kufanyia kazi madhara yatakayo tokana na utekelezaji wa mradi wa EACOP,

(e) uhamasishaji wa maendeleo yenye manufaa kiutamaduni,

(f) Kushirikiana ipasavyo na serikali,

Utekelezaji wa ahadi za EACOP utaeleza katika Mpango unaofuta wa mradi, ambao utahusisha wasifu wa kina wa jamii zinazopitiwa na mradi, pamoja na wasifu mahsusi wa jamii ya waakie wa Napilikunya.

## Ridhaa ya jamii kwa kazi za mradi wa EACOP

Jamii ya wa-Akie wa Napilikunya inaridhia kufanyika kwa shughuli za mradi wa EACOP katika jamii yao wakati wa maendelezo, ujenzi na utekelezaji wa bomba la mafuta. Kupitia utaratibu wa shirikishi wa ushauri na jamii ya wa-Akie and viongozi wa kimila, EACOP itatatua matokeo hasi yatakayotokana na shughuli za mradi na itatekeleza faida za kimaendeleo katika njia inayoheshimu mila na desturi . EACOP itasaidia kwenye juhudi za kuwanjegea uwezo jamii ya waakie ili waelewe na kushiriki katika kazi za mradi kwa viwango vya FPIC. EACOP pia itabuni njia ya utatuzi wa migogoro inayoendana na utamaduni wa waakie na na kuishirkisha serikali ipasavyo.

## Ridhaa ya Jamii Kuhusu Kuhamishwa kwa Eneo la Kuabudia

Ridhaa ya jamii kuhamisha eneo la kuabudia Kwa kuzingatia u-maalum wa changamoto za jamii ya Akie, na uwezekano wa mradi wa EACOP kuathiri maeneo yao ya kuabudia, makubaliano haya yana ainisha majadilino ya nyongeza na ridhaa iliyofikiwa na jamii ya Akie kwa ujumla kuhusu kuhamishwa kwa eneo la kuabudia.Hapo awali, eneo la kuabudia lilikwa chini ya Mbuyu uliopo katika ardhi ya familia ya Lembulu. Eneo hilo la kuabudia kwa sasa litahamishiwa katika ardhi ya familia ya Orng'idi. Eneo hilo la kuabudia lina umuhimu wa kipekee kwa mila na ibada za jamii ya Akie kwa ujumla. Hivyo basi kulikuwa na umuhimu wa kuwa na makubaliano mengine mahususi na jamii ya Akie kwa ujumla. Undani wa majadiliano ya awali uliozingatia mil ana desturi, na namna ya uamishwaji wa eneo la kuabudiwa ume nakiliwa katika muhutasari wa mikutano na ripoti zilizoandaliwa na mshauri wa EACOP kuhusu haki za jamii za pembezoni zinazo jitambua kama jamii za asili, Dr. Elifuraha Laltaka

(Mtaalam wa Kitazania wa maswala ya jamii za asili). Nyaraka hizo zime ambatanishwa katika makubaliano haya na kuitwa Nyongeza A.

## Ridhaa ya Jamii Kuhusu shughuli kufanyika karibu na msitu

Pamoja na kwamba mradi wa EACOP hauathiri moja kwa moja msitu-tengwa wa jamii ya Akie ambao jamii ya wa Akie inautegemea kwa Maisha yao na kwa ajili ya ibada, kumekuwepo na ushirikishwaji wa awali kabisa kwa jamii nzima kwa kuwa shughuli za Mradi zitapita karibu na msitu huo. Ushirikiswaji huo pia ulihusisha uhakiki uliofanywa na Dr. Laltaika ambao ulijikita katika kuhakiki namna jamii ilivyo kubali kuwepo kwa shughuli za EACOP kwa mujibu wa FPIC kabla ya kusainiwa kwa makubaliano haya. Muhutasari wa ushirikishwaji huo umeambatanishwa na kuitwa Nyongeza B.

## Muda wa Kupatikana kwa Ridhaa

Muda wa utiaji sahihi wa makubaliano haya kabla ya kukamilishwa kwa mpango kazi wa EACOP uliombwa na jamii ya Akie ili kuheshimu ratiba zao za kimila za kufanya matambiko ya kuhamisha eneo la kuabudia na kuridhia makubaliano (kabla ya msimu wa kiangazi).

## Ushirikishwaji wa wawakilishi wa mashirika yasiyo ya-kiserikali (NGOs)

Ili kuhakikisha kwamba mchakato wa kupata ridhaa ya FPIC unazingatia tunu za FPIC kwa mujibu wa mila na desturi za Tanzania, na kwamba ridhaa ya jamii imepatikana bila shuruti au ushawishi wa EACOP ama mdau mwingine yeyote, ridhaa hii ya FPIC ilijadiliwa katika vikao kadhaa vya jamii kwa msaada wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) zinazo saidia kazi za EACOP. Vilevile, utiaji sahihi wa makubaliano ya FPIC yameshuhudiwa na Dkt. Laltaika mbele ya NGOs na wawakilishi wa serikali.

## Uteuzi wa wawakilishi wa jamii

Wawakilishi wanne wa jamii wamechaguliwa kwa uhuru kwa mchakato wa ushirikishwaji wa wanajamii ya Akie kwa ujumla, wakiwemo wanawake na vijana ili watie sahihi kwa niaba ya Jamii ya AKie kwa ujumla.

## Utiaji wa Sahihi